
## Dira

Taifa lenye Umwagiliaji endelevu unaochochea mapinduzi ya kilimo.

## Dhima

Kubadilisha kilimo kupitia uratibu, udhibiti na uendelezaji wa Umwagiliaji endelevu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.





***"Kilimo cha Umwagiliaji, Kilimo cha Uhakika"***


**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

**S.L.P. 146, Njedengwa, Dodoma**

**Simu:**
+255 26 296 2073

**Barua Pepe:**
info@nirc.go.tz

**Facebook/Instagram/Twitter:**
Nirc_tz

**Youtube:**
Tume ya Taifa ya Umwagliaji

**Tovuti:**
www.nirc.go.tz


# MAJUKUMU YA TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**



## MAJUKUMU YA MSINGI YA TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI NI:

- Kuratibu
- Kuendeleza na,
- Kusimamia maendeleo ya sekta ya Umwagiliaji nchini.



## MAJUKUMU MAHUSUSI YA TUME NI KAMA IFUATAVYO:

**A/** Kuishauri Serikali katika utekelezaji na kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, Mkakati wa Maendeleo ya Umwagiliaji, Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji na Sheria ya Taifa ya Umwagiliajia

**B/** Kuwakilisha Serikali kwenye mikutano ya kitaifa na kimataifa katika masuala yote yanayohusu uendelezaji na usimamizi wa kilimo cha Umwagiliaji.

**C/** Kuratibu shughuli zote za Umwagiliaji katika sekta ya umwagiliaji zinazotekelezwa na washirika au wadau wengine wa maendeleo;

**D/** Kuhamasisha na kudumisha ushirikiano na taasisi za kimataifa zenye kutekeleza majukumu yanayofanana na Tume katika masuala ya Umwagiliaji;

**E/** Kupanga, kufanya pembuzi yakinifu na usanifu, kujenga na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya Umwagiliaji;

**F/** Kuanzisha na kuendesha vituo vya ukodishaji wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kuisaidia Sekta binafsi kuwekeza kwenye kilimo cha Umwagiliaji;

**G/** Kusajili na kutunza orodha ya wamwagiliaji;

**h/** Kuhamasisha na kudumisha mahusiano na taasisi zinazotoa programu za mafunzo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali watu kwa madhumuni ya kupata wataalamu katika sekta ya Umwagiliaji;

**I/** Kuwa jukwaa la kubadilishana uzoefu na kupashana habari katika masuala ya Umwagiliaji;

**J/** Kujenga uwezo wa wamwagiliaji kwa ajili ya kuongeza ushiriki wao katika kupanga, kutekeleza, kuendesha na kusimamia skimu za Umwagiliaji;

**K/** Kufanya na kuratibu tafiti, kusambaza teknolojia sahihi zitokanazo na matokeo ya tafiti na kutoa msaada wa huduma za kitaalamu kuhusu Umwagiliaji;

**L/** Kuhamasisha uendelezaji wa mabwawa kwa ajili ya matumizi ya Umwagiliaji na shughuli nyinginezo za kiuchumi na kijamii;

**M/** Kusimamia masuala yote yanayohusu maendeleo ya Umwagiliaji na ushirikiano na wadau mbalimbali katika maendeleo ya Umwagiliaji;

**N/** Kuidhinisha ujenzi wa mifumo ya umwagiliaji, kusimamia viwango na miongozo kwa ajili ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za Umwagiliaji;

**O/** Kuhamasisha matumizi ya maji yenye ufanisi katika mifumo ya Umwagiliaji na kuhakikisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji kwa maendeleo ya kilimo cha Umwagiliaji;

**P/** Kuishauri Serikali katika masuala yote yanayohusu maendeleo na uendeshaji wa sekta ya Umwagiliaji nchini;

**Q/** Kutekeleza majukumu yote muhimu katika kuendeleza kilimo cha Umwagiliaji.

